REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 6th March, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 9.20 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

PAPERS LAID

QUARTERLY REPORTS, CFSP, CFSP PUBLIC PARTICIPATION REPORT, DMSP & ASSEMBLY CALENDAR

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker. Hon. Speaker, on behalf of the Majority Leader who has delegated House Business to me for now, I want to table the following papers

a) Quarterly reports and Financial Statements for the period ended December 2023.

b) Public Participation report on the CFSP 2024 by the department of Finance, Economic planning and County Development.

c) The County Fiscal strategy paper (CFSP) 2024 by the County Government of Laikipia.

d) The County Debt Management Strategy Paper 2024 by the County Government of Laikipia.

e) Calendar of the Assembly for the Third session.

(Hon. Stephen Ndiritu laid the papers on the Table)

Speaker: Thank you, Honourable Members. Thank you, Hon. Stephen for the Report and Papers that you have laid. I want to commit;

The Quarterly reports and financial statements for the period ended December 2023 to all Sectoral Committees and Public Participation report on the CFSP 2024 by the department of Finance, Economic planning and County Development.

The County Fiscal strategy paper (CFSP) 2024 by the County Government of Laikipia and equal The County Debt Management Strategy Paper 2024 by the County Government of Laikipia committing them to the Budget Committee.

Thank you.

NOTICES OF MOTION

COUNTY ASSEMBLY CALENDER

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Mr. Speaker. I want to give notice of the following motion;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

THAT, pursuant to Standing Order No. 29 (1), this Assembly approves the Calendar (Regular Sessions) for the Third Session of the Third County Assembly (February to December, 2024).

Thank you.

MOTION

COUNTY ASSEMBLY CALENDER

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker. On behalf of Majority Leader, I beg to move the following motion;

THAT, pursuant to Standing Order No. 29 (1), this Assembly approves the Calendar (Regular Sessions) for the Third Session of the Third County Assembly (February to December, 2024). Asante, Bwana Spika.

Huu ni muswada ambao tunataka kuleta Bungeni. Ni muswada ambao tunafaa kujadili kama Bunge na kuhakikisha ya kwamba zile biashara tunafanya tukija hapa, ni ambazo zinatambulika na wananchi. Vilevile, ni siku ambazo ziko katika kumbukumbu la Bunge hili.

Ni vizuri Bwana Spika, niweze kukumbusha hawa Waheshimiwa wenzangu ya kwamba kama hatutakuwa na Kalenda, ni kumaanisha hakuna siku ya kuingia Bunge. Kwa hivyo, wale ambao tuko hapa, tuko na jukumu la kujadiliana, kuongea na kusikilizana tupitishe hili Kalenda.

Hii Kalenda inatuongoza kutoka mwezi wa Februari wakati ambapo tulipokuja hapa mpaka wakati ambapo tutakapofunga. Tutakapoelekea Krismasi kusherehekea pamoja na watoto wetu na familia zetu, na hata Yesu Kristo atakapozaliwa wakati wa Desemba, itakuwa ni jambo la busara kama sisi wote tutashikana tukiwa Waheshimiwa kutoka sehemu mbalimbali tukiwa vyama vyote.

Wale wote tuko hapa tuungane maana hii Kalenda si ya Chama moja wala kingine, bali inatuongoza sisi wote milengo yote. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, ningewaomba hawa Waheshimiwa wenzangu tuweze kuangalia hii Kalenda.

Bwana Spika, naweza kuhakikishia wenzangu ya kwamba, Kamati ya Utendakazi wa Bunge wamekaa chini na wakaangalia hii Kalenda. Walikuwa na siku maalum ya kuiangalia na kujua ya kwamba tunapoanza Februari 13, tutakuwa tumeenda wiki kadhaa kisha, tutapumzika Aprili siku ya Jumatatu mwaka wa 2024. Hicho ndicho kitakuwa kipindi cha kwanza.

Kamati ya Utendaji wa Bunge wameweza kuangalia majukumu ya Waheshimiwa. Bwana Spika, tukiwa Bunge pia tunawakilisha wananchi ambao wametupatia nafasi huko mashinani. Kama hatutakuwa na mapumziko kidogo, huenda sisi kama Wabunge ambao tunawakilisha wananchi hapa tukakosa nafasi ya kuongea nao na kujua yale matatizo yanayowakumba na kujua yale mambo ambayo wangetaka tuwe tunawatetea .

Kwa hivyo, Bwana Spika na Waheshimiwa wenzangu, kutoka Februari mpaka Machi tarehe 28, hapo tutakuwa tukifanya kazi ya Bunge kisha tutapumzika kutoka tarehe hiyo ambayo nimetaja.

Kwenye sehemu ya pili, tukienda tutarudi tena Tarehe 16 Mwezi wa nne. Kuanzia hapo tutafanya kazi bila kuchoka. Tutajikakamua vya kutosha kufanya kazi ya Bunge hadi tarehe 24 Juni. Baada ya hapo tumeona ni vizuri tuwe na mapumziko kidogo, turudi kwa mwananchi na kuongea naye ili atupe mawaidha na yale mambo anayotaka tuyazungumze.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Vilevile, Mheshimiwa Spika, ni vyema kuelewa kuwa Wabunge wengine wanatoka mbali. Wengine wanatoka Magharibi, wengine Kaskazini, na wengine tuko Mashariki. Baadhi yetu hatuna nafasi ya kuwa na familia zetu kuanzia Mwezi wa Kwanza hadi wiki ya mwisho. Ndiposa tumeona ni vizuri tuwe na nafasi ili wakati huko Bungeni, basi uwe na familia kwa sababu baadhi yetu ni wazazi. Hata hawa wafanyikazi ni wazazi na tunapokuwa hapa, wana kazi nyingi ya kufanya kuhakikisha kuwa wanatushughulikia.

Mheshimiwa Spika, tunaye Mheshimiwa Kamara ambaye ametoka upande wa Magharibi. Akiwa hapa anakaa wiki nzima bila kumwona kijana wake ampendaye. Akiwa na hiyo nafasi ya wiki moja au mbili ataweza kufika pale na kuonana na mtoto wake, azungumze na mke wake na wapange mambo mengi. Tulisikia tukiwa kwenye mkutano huko Naibu wa Rais akituambia ni vizuri tuongeze kura katika eneo letu la Mlima Kenya.

Ni vizuri niseme hivyo hawa Waheshimiwa wengine wakiwa hapa kwa sababu ilikuwa wazi. Sisi tumepunguza kura sana. Wakati huo tutampa nafasi Mheshimiwa Kamara na wale wengine walio na damu moto wafanye majukumu. Mheshimiwa Wachuka alisema tumefungua chumba cha uzazi lakini hakuna watoto wanaozaliwa. Huu ni wakati wa akina Kamara, Lempaira, Tony, Salim (sijui kama yupo), na Shuel kuhakikisha kuwa hii kazi imefanyika tuongeze kura. Tumeangalia kila mahali kuhakikisha kila kitu kinaendelea vizuri na hakuna mahali tunapotaka kufanya mambo visivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu ya tatu itakayoanza Septemba hadi Oktoba. Halafu kuna sehemu ya tano itakayoanza Novemba mwaka huu hadi tarehe kumi Februari mwaka wa 2025. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawaomba wakati huu tusikizane kwa huu mswada ambao umetengenezwa na Kamati ya Shughuli za Bunge ambayo imepewa majukumu na Kanuni za Bunge na Katiba kupanga biashara za Bunge. Nataka kuwahakikishia ya kwamba wameangalia kila kitu, na walio kwenye hiyo kamati ni watu wakakamavu, wenye haki na wanaoangalia maslahi ya Wabunge wote ili kila kitu kiendelee vizuri.

Kwa hivyo, nawaomba hawa Wabunge wote kwa heshima tuungane kuupitisha huu mswada ili Bunge liwe na nafasi ya kufanya kazi. Tukipitisha huu mswada, utachapishwa kwenye Gazeti rasmi la Serikali na mwananchi aliye kwenye kijiji cha Maina, Matanya, hapa Majengo, Chumvi na Sosian atajua siku ambazo tunafanya biashara. Akipata nafasi atakuja hapa kuangalia vile tunafanya na kuhakikisha ya kwamba kazi tuliyopewa inafanyika. Nawaomba nyinyi Wabunge, tuunge mkono huu mswada na kwa sababu ni mswada ukatao kila mahali, namweleza Mheshimiwa Salim ambaye ni mgeni kwenye hiyo kamati, achangie kwenye huu mswada na kuuafiki ili tuwe na kalenda ya Bunge na tuipitishe. Asante.

Hon. Salim Edung: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipa hii nafasi. Naunga huu mswada mkono kwa sababu hakuna kazi inaweza kufanyika bila mpangilio. Ukiangalia hususan mashinani, tunapokuwa katika Bunge hili, lazima pia tuwe na njia au mikakati kwamba leo tuko Bungeni na siku hiyo nyingine tuko mashinani kuona miradi inayofanyika. Ukiangalia taasisi mbalimbali, hususan elimu, kwenye shule kuna ratiba ya kila somo, kwa mfano leo kuna hisabati na kesho kuna Kiingereza. Vilevile, kwenye hili Bunge lazima tuwe na mwongozo wa kutuongoza katika mikakati ambayo tunafanya katika hili Bunge.

Tusipokuwa na mwongozo, hiyo biashara haitafaulu. Hata anayeuza duka mashinani au mjini lazima aweke mikakati ili duka lake liende mbele. Kwenye Bunge hili pia, lazima sisi tuwe na mikakati ya kusema kuwa shughuli yoyote inayofanyika kwenye hili Bunge inahusu wananchi wa Laikipia. Lazima tuwe na mikakati na mipangilio. Tunapopata likizo tunahitaji kuenda mashinani tuone miradi iliyo pale, yenye imetekelezwa na yenye haijatekelezwa, na tujue kama hio ni mipango tuliyoweka kwenye hili Bunge.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Kusipokuwa na miradi inayofanywa mashinani, basi sisi tutakuwa tukiangalia nini? Inafaa kila kitu kiwe na mipangilio. Hata kwenye shule watoto hupewa likizo. Ifikapo Mwezi wa nne wanapewa likizo waende wapumzike, waende nyumbani kukutana na familia zao, na wazazi waangalie waliyokuwa wanayafanya shuleni. Vilevile, katika hili Bunge, tunapopata likizo ni nafasi ya kukutana na wananchi kule mashinani, kujua shida walizo nazo na kuangalia miradi ambayo imefanyika na yenye haijafanyika, ili tunaporudi kwenye hili Bunge tuwe na jambo la kuongea kuhusu, kwamba kwenye eneo fulani kulikuwa na jambo hili ama lile.

Ndiposa sisi kama Waheshimiwa katika Bunge hili tuko na majukumu ya kujua ni nini kinafanyika huko na nini hakijafanyika na ninaunga mkono. Pia katika Bunge hili, tusipokuwa na kalenda tutakuwa tumepea Bwana Spika kazi ngumu. Sisi ndio tunapanga zile kazi zinafanyika katika Bunge hili na ndio kila kitu iende sambamba. Kwa hayo machache, naunga mjadala huu mkono. Asante sana.

(Question proposed)

Hon. Paul Leshuel: Thank you Mr. Speaker. I also stand to support the motion. In this House of Law, we must have a plan. According to the Standing Orders and the laws of this country, the County Assembly must have a calendar so that everybody will understand that Members are in the Assembly for a specific period.

As we know in the Assembly, there are many interested parties from the public to see what is happening, the Assembly proceedings and understand what Members do. If you fail to plan, you plan to fail. We must have a plan.

The other thing, as you know our plan and role, we must be here to make laws and oversight the Executive. We need time to oversight and go to the ground to make sure whatever the Executive is passing is what has been passed in this House. We have a big role in planning so that we can achieve whatever we want to do. I support.

Mr. Speaker, I know the importance of it and we must all support so that we know when we are supposed to be here and when is recess. When we are here, our people from the wards are missing us because we are not available there. We must get a chance to go back to the community and get their views so that when we come back, we are able to come up with plans that will make them happy. I also agree with Members that we must work together.

According to the County Government Act, 2012, we have two Arms of the Government so that we can have checks and balances. The moment we allow the Executive to do what they think is right, it might go the other way. There must be checks and balances. It is our responsibility especially as an Assembly to see what we pass here as laws is implemented accordingly. It is also our responsibility to work together and make sure we have served Laikipia. I support. Thank you.

Hon. Nicholas Mwaniki: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support this motion. This is timely and having a schedule of the sittings is paramount because we have planned ahead on this Financial Year. I want to congratulate the House Business Committee for work well done. I can see we have long and short recesses. This where we play the role of oversight of projects and we get the views of the public on what should be done on the ground. These are checks and balances that we need to achieve so that we get tangible developments.

Mr. Speaker, I can see we have sittings Tuesday, Wednesday and Thursday that we will be committed here in the Assembly as we draft and pass laws in this House. Having this schedule is good but as we plan ahead, we had a proposal previously of having the sittings of this House for two days so that we can be able to commit the Committees on the oversight. The

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

key thing we are doing for our people is service delivery. The more we budget for the funds of this county, the more we roll out projects on the ground through the Executive the more we have a bigger role on oversight.

As we move on, I think we need to have a discussion so that the House Business Committee can plan on how change the Standing Orders of this Assembly. We have two days in this Assembly and three to play the role of oversight on the projects on ground. As I support, there is still a role the Assembly and Committees need to play because the committees need to be more active and effective on the ground. Thank you. I support.

Hon. Benson Kuria: Bwana Spika, nashukuru sana kwa hii nafasi ambayo umeweza kunikabidhi. Naunga mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Ndiritu mkono. Naunga nikijua ya kwamba ni mwelekeo mpya wa huu mwaka wa 2024.

Bwana Spika, ninaona ni vyema kwa sababu kuna wale ambao wanaotuwakilisha kwa biashara za Bunge hili wakiongozwa nawe Bwana Spika na kamati yako. Mimi nimeweza kuletwa katika hili Bunge na chama cha UDA ambacho kinaongoza Jamhuri ya Kenya. Niko hapa kuunga miswada yote ya serikali mkono ili tuweze kuona ya kwamba kile ambacho serikali itakachopanga, kitawezekana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuambia Waheshimiwa wenzangu, kwa sababu sisi huwa tunapangiwa biashara za Bunge na Waheshimiwa wenza, ningetaka kuwasihi kwa sababu ukisoma katika biblia kitabu cha Mathayo 5:8, inasema heri wenye moyo safi maana watamuona Bwana. Kumuona Bwana ni kuwaona wananchi wa Laikipia. Kama Kamati ya HBC watakuwa wamepanga ya kwamba hatutakuwa tukihudhuria Bunge, ni kumaanisha ya kwamba sisi sio watiifu.

Mimi nisiwe wa kwanza kufanya hili Bunge ikose akidi. Hivi leo ninajua ya kwamba yale yatakayo tendeka nikiwa nimepangiwa na wale ambao tumechagua, nikiwa sihudhurii Bunge kwa sababu moja ama nyingine, sitaweza kuona wananchi wa Jimbo la Laikipia. Kwa hivyo, ningependa kuwasihi Waheshimiwa kwa sababu aliyekufanya uwe hapa, Mheshimiwa Anthony Theuri, ni wananchi wa Wadi ya Nanyuki.

Kwa hivyo, ni kumaanisha ya kwamba tusipokuwa na akidi katika hili Bunge, wale wananchi watatutazama. Siku ambayo wataenda kukuangalia, watasema ya kwamba tulikutuma lakini haukutuwakilisha, tulikupatia nafasi lakini ulituangusha. Kwa hivyo, ningependa Waheshimiwa wenza tuweze kuunga mkono huu mswada ili tukirudi kwetu, wananchi wakaweza kuona ya kwamba kuna watu ambao wanaowakilisha kwa njia mwafaka kabisa. Kwa hayo mengi, nashukuru kwa wale ambao wameketi na kusema.

Ninaunga 100% na Mheshimiwa Ndiritu, uendelee hivyo hivyo ili wakati utakaporudi Thingithu, utakuwa na jambo la kusema. Kama hautahudhuria vikao ambazo zimepangwa ambazo tunajadiliana sasa hivi, watasema ya kwamba tulikutuma lakini haukutekeleza, tulikuambia lakini haukufanya. Asante.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. Kwanza nikushukuru Waheshimiwa wenzangu na pia nakushukuru kwa vile mlitembelea wadi yangu kutoka Jumapili hadi Jumatatu. Nashukuru pia Kamati ya HBC ambao wameketi chini na kuangalia mambo ya kalenda yetu. Kama vile nimekuta Mheshimiwa Stephen akiongea, Bunge ambalo halina mpangilio sio Bunge. Mpangilio katika hili Bunge ni kupanga mambo ya kalenda na kalenda ndiyo hutufanya tuwe hapa. Wakati hatuko hapa hata kama ni wiki mbili, sisi huenda kuonana na Wanjiku.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Mimi nililetwa hapa na watu wa Wadi ya Igwamiti na pia wenzangu wameletwa hapa na vyama mbali mbali kama vile ODM na UDA na Hao ni wafanyikazi. Chama kilikaa chini kikaona ya kwamba yule mtu ambaye aliletwa hapa na ODM kwa kuteuliwa yuko na jukumu sawa na mimi. Katika serikali iliyopita, nilikuwa nimeletwa hapa na chama cha Jubilee. Niling'engana na kupata nafasi katika hili Bunge tena kwa kuchaguliwa. Kwa hivyo, sisi wote ambao tuko hapa tuko na jukumu la kufanyia Wanjiku kazi.

Kama vile mwenzangu Mheshimiwa Benson Kuria amesema, kuna maswali ambayo tutaulizwa na wananchi na kama wananchi hawatauliza, kuna Mungu juu mbinguni ambaye atauliza. Mimi napata mshahara lakini sitekelezi mambo yanatakiwa. Hili ni Bunge la sheria. Kama jana sikuja katika Bunge kwa vile nilikuwa nimefanya kazi ngumu kwa wiki mbili zilizopita. Jana nilishindwa kwa sababu nilikuwa naumwa na kila kona ya mwili lakini leo ni lazima nikimbie hapa ili Wanjiku asione ya kwamba alinipatia jukumu lakini naonekana Igwamiti tu nikiranda randa.

Katika hili Bunge, hata kama sipendi Mwaniki, sio mimi ambaye nilimleta hapa, aliletwa na watu wa Tigithi. Kama sipendi Theuri, Theuri aliletwa na watu wa Nanyuki. Kama sipendi Shuel, aliletwa na watu wa kutoka kwake. Kwa hivyo, wakati ambao tuko katika hili Bunge, wacheni tufanyie Wanjiku ambaye alituleta hapa kazi. Tushukuru pia serikali yetu ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Ruto na naibu wake Mheshimiwa Rigathi Gachagua kwa kazi nzuri ambayo wanafanya.

Tunasema ya kwamba tunaunga mkono Rais wetu kama vile alisema ya kwamba kama Raila anaweza enda na apewe kiti huko, sisi hatuna shida kwa sababu yeye ni mwana Kenya. Akipewa kiti huko sisi hatuna shida kwa sababu yeye ni Mkenya. Nashukuru sana na ninaomba Waheshimiwa wenzangu tuchangie haya mambo ya kalenda na HBC tunawashukuru. Wakati mtapata kikao kingine, mkumbuke kuna jambo ambalo tulikuwa tumeuliza ya kuhudhuria Bunge siku mbili kwa wiki.

Baada ya kuona Wanjiku, tunarudi katika hili Bunge na kuleta yale ambayo tumetoa mashinani. Unapoona Rais pale, unaona serikali yote na katika hili Bunge lazima tuheshimiane. Nikiona Leila pale, nione mwenzangu na nikiona Theuri pale, nisione kama mtoto wangu lakini nimuone kama mtu aliyechaguliwa na watu wa Nanyuki na yeye ndiye husema hapa Nanyuki. Ukija pale Igwamiti, ukumbuke umepata Irene Wachuka John AKA Mama yao.

Ninashukuru wale ambao walikuja huko na ninauliza kina Mheshimiwa Gathoni, Leila, Eunice, Kihika, Kamala Mwaniki na wengineo mulete Watoto kwa sababu muko na damu moto. Usiende huko Nairobi kwa sababu sasa tuko na chumba cha kina mama ya kisasa. Wale ambao walikuwa wameingia pale waliweza kuona ya kwamba huko ni kama Hospitali ya Nairobi. Nashukuru serikali ya Gavana Irungu kwa vile alirudisha wale madaktari arobaini. Nikufukuza mtoto wa Theuri leo, kesho wangu naye atafukuzwa. Ninaunga nikisema ya kwamba watu wanafanya kazi kama timu. Usiseme ya kwamba hautaenda Bungeni. Kuja ili tufanya kazi Pamoja kwa sababu nyumba ambayo hufanya maombi Pamoja, kuna Mungu katikati.

Bwana Spika, sisi tunakuombea utuongoze vizuri, tuko nyuma yako na serikali ya hili Bunge. Kila mtu yuko na kazi yake. Wale ambao wamechaguliwa katika wadi kumi na tano, tuko na kazi ngumu sana mashinani. Wale ambao waliletwa na hivyo vyama viwili, UDA na ODM, hapa hakuna vyama.

Tukifika hapa ni kufanya kazi. Mheshimiwa Umija, fanyeni kazi na hapa hatuna chama. Sisi tukiingia hapa tuko Bunge moja kwa hivyo, tufanye kazi pamoja kama timu. Katika Bunge hili, sisi ni mandugu na madada. Kwa hayo machache ama mengi, Mungu awabariki. Asanteni.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Hon. Anthony Theuri: Asante sana, Bwana Spika. Nasimama kuunga mkono mjadala ambao umeletwa na Rafiki yangu Mheshimiwa Ndiritu. Utaratibu ni mzuri na Biblia inatuambia vizuri sana kama vile Mheshimiwa Benson ametuelekeza katika Biblia kwamba Binadamu hupanga, lakini Mungu ndiye hutimiza. Huo mpangilio uko sawa na ninaomba kwa sababu imetengenezwa na wenzetu ambao tunaunga mia kwa mia. Ni vizuri kwa sababu hawapangi ili wakose kuja.

Hivyo mmepanga ni kuonyeshana kwamba huo ndio utaratibu ambao tutafuata. Tutafuata hilo na vilevile ni vizuri nimkumbushe rafiki yangu Mheshimiwa Kamara kwamba Biblia ni moja na wakati unanukuu, ni vizuri unaielewa vizuri. Umesema Matayo tano mstari wa nane inasema ya kwamba, 'ni heri wenye mioyo safi'. Kwa hivyo ,tusimame na hayo maandiko.

Ni vizuri nikukumbushe kwamba Kitabu cha Yeremia kumi na saba mstari wa tano, Mungu ndiye huchunguza roho ya mtu, anajua matarajio na anakuja kulipa. Kama uko na roho nzuri hauhitaji kutuambia. Ninaomba Mungu akusaidie uwe na roho nzuri tukiwa pamoja kwa sababu sijui ni kwa nini ukasimama na kutumia mfano mbaya na mimi. Ni kwa nini usitumie mfano mzuri kwamba watu wa Nanyuki wanasimama na kufanya kazi nzuri.

Ningeomba kama ni lazima utumie mfano, tumia mfano mzuri kwa sababu maneno yako na nguvu. Wewe ni Mheshimiwa mkubwa kuniliko, ni vile hujawahi jielewa kwa sababu umechaguliwa Laikipia yote. Ukiwa Nanyuki wewe ni Mheshimiwa, ukiwa Thingithu wewe ni Mheshimiwa na ukiwa Igwamiti, wewe ni Mheshimiwa. Mimi nimeletwa kilomita nne mraba, kwa hivyo wewe, ni Mheshimiwa kila wakati.

Wakati unasimama, uko na nguvu kutuliko. Ukisimama Nanyuki, wakilisha vizuri na ukisimama Mirigwet, wakilisha vizuri. Kwa hayo machache ama mengi, tuwakilishe. Nafurahi sana kwa sababu leo kuna akidi. Mheshimiwa Spika, jana tulikuwa na wewe hapa tukipeana hadithi. Kwa sababu leo kuna utaratibu, ninaamini kwamba kwa siku zijazo tutapata biashara na tutaweza kuelekeza Kaunti yetu mbele. Asante, Mheshimiwa Spika. Naunga mkono.

Hon. Nicholas Lempaira: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii nafasi ili nichangie mjadala wa siku ya leo ambao tunaunga mkono asilimia mia kwa mia. Tunapongeza kamati ambayo imekaa chini na kuweza kutoa huu utaratibu. Bwana Spika, ninaposikia wenzangu wakiongea, ni vizuri kusikiza vile wanasema. Pia ni vizuri niwakumbushe ya kwamba jana Mheshimiwa Theuri ameonja uzuri wa kuja Bunge peke yake.

Aliweza kuhisi vile huwa tunahisi asipokuja Bunge. Hivyo ndivyo huwa tunasikia ukija mara moja na kupotea. Bwana Spika, ningependa kuunga mkono vile wenzangu wamesema ikiwezekana tuweze kuendeleza shughuli za Bunge kwa siku mbili kwa wiki. Itakuwa ni vyema tukija Jumanne na Jumatano ili siku hizo zingine, tupatiwe nafasi ya kurudi mashinani ili tuweze kufanya kazi ya uangalizi ambayo ndio iko. Kwa hayo, naunga mkono. Asante.

Hon. Catherine Umija: Asante sana, Bwana Spika kwa kunipatia hii fursa. Ninaunga mkono kalenda ya huu mwaka. Natumaini kwamba Wabunge wenzangu tutakuwa tunakuja katika Bunge. Tuko na ratiba mwafaka na tuko na muda wa kupumzika na kwenda kufanya kazi ambayo tutahudumia wananchi na familia zetu. Natarajia ya kwamba miswada ikija katika Bunge, tutasaidia wananchi.

Ninahimiza Wabunge ya kwamba tunahitaji miswada mingi katika Bunge. Tuko na wakati na ni sasa. Kama hatutafanya, tutasaidiwa na wengine. Shukran.

Speaker: Thank you, Hon. Catherine Umija. I now take this opportunity to invite the mover of the motion to reply.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nasimama hapa kuwapongeza Waheshimiwa wote kwa kuchangia huu mswada na vilevile kuunga mkono bila kutoa sehemu moja ama ile ingine. Sisi tuko tayari kufanya kazi kwa sababu tulipatiwa kura na kila mtu alipewa jukumu la kuja hapa kufanya kazi. Naomba tufanye kazi kwa umoja. Kama vile mmesema, kila mtu ataulizwa maswali na wananchi ambao walimchagua.

Ninajua hakuna mtu hapa ambaye hakupata kura na hakuna mtu alifika hapa bila kuwa na njia ambayo alipitia ili afike hapa. Itakuwa ni jambo la busara kama sisi zote tutaungana na tufanye kazi vizuri. Mahali ambapo tunafaa kufanya biashara, tufanye biashara. Mahali ambapo tunafaa kupumzika, tupumzike. Mahali ambapo mtu anafaa kufanya kazi yake, afanye kazi yake.

Kama vile Mheshimiwa Leshuel amesema, hata vita ikija, walimane kwa sababu hakuna mtu yuko na mtoto kwa mgongo bali ni kulimana mpaka dakika ya mwisho. Kwa hivyo, ninaomba tukiwa hapa tufanye biashara na tufanye kazi kwa njia ambayo inafaa. Ningetaka kumwambia Mheshimiwa Leshuel tuko hapa kufanya kazi na tutafanya. Ninashukuru kwa vile mmechangia mswada kwa njia ambayo inaeleweka.

Hapa tuko na nafasi ya kufunga Bunge na ya kuja kufanya kazi. Wale ambao wako na miswada, ningeuliza kamati zote haswa wale ambao wanajua wako na ripoti ambazo wanafaa kuleta katika Bunge, wafanye hivyo kwa haraka na upesi. Sisi kama kamati tuko na shida ya kupanga biashara lakini tukienda kwa ripoti ambayo imetayarishwa ya kuonyesha vile biashara ziko, kila kamati iko na biashara.

Kamati ambayo inaongoza kwa kuwa na biashara mingi ambazo hatujui zitatufikia lini ni CPAIC. Wale ambao wako kwenye hiyo kamati wako na jukumu na tumewapatia Kalenda. Nyinyi ambao mnapitisha naona nyuso zenu zinakaa kupitisha. Kama vile naona nyuso zenu, tuko kwenye kiwango cha kupitisha hii biashara. Kama vile Mheshimiwa Wachuka amesema, mahali kuna mapumziko, watu waende wakafanye kazi vile ambavyo inastahili.

Ametufungulia chumba cha uzazi kwa hivyo, mtengeneze kazi. Juzi alituambia tufanye kazi yetu kama wanaume. Kwa hivyo, wanaume mkienda huko hakuna kuregarega. Fanya kazi kama vile unafanya hapa Bunge. Hakikisha kuna akidi na kila kitu iko sawa. Kwa machache, nashukuru Waheshimiwa na tuweze kufanya kazi kwa njia ambayo inafaa. Asante sana na Mungu awabariki.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until later today Wednesday 6th March, 2024 at 2.30 p.m.

The House rose at 9.45 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*